1st ed

# JOGRAFIA.

MWANANGU.—Nitakwambia elimu ya Jografia. Usikie ana nisemavyo, baadaye nitakuuliza maswali, naswi tuta-andika maneno ya kukumbukwa.

Jografia hutwambia mambo ya uso wake dunia tunayekaa. Dunia inaviringana kama chungwa, inayo inchi na maji, na maji hupita marra mbili eneo la inchi. Dunia ni kubwa sana, hugeukageuka sikuzote. Dunia hugeuka kama pia, nayo teua huzungukazunguka katika jua. Hapana kitu chini yake, wala haina hatari ya kuanguka.

Labuda umethani inchi ni pana na sawa, imetulia sana, na inchi pana kuliko bahari.

Vitu havinavyo sikuzote kama vilivyoonekana. Utauliza labuda, Tupateje kujua kama dunia imeviringana? Kwanza, watu wameizunguka katika merikebu. Ya pili, merikebu zikitoka pwani, hutoweka kidogo kidogo, na sehemu iliyo chini hutoweka kwanza. Ya tatu, mwezi ukipatwa, kivuli cha dunia kinaonekana juu ya mwezi, na kivuli hiki kimeviringa.

## I.

S. Jografia hutufundisha nini?

J. Jografia hutufundisha mambo ya uso wake dunia.

S. Namna yake dunia nini?

J. Dunia imeviringana kama chungwa, si kama pesa, wala si kama yayi.

S. Dunia inayo nini?

J. Inchi na maji.

201. g. 228

1878

Digitized by Google

S. Husimama juu ya nini?

J. Haina kitu chini yake. Ni planeto, ao sayari, ndiyo nyota isiyotulia.

S. Yaendaje dunia?

J. Dunia huzunguka katika jua, na hugeuka tena yenyewe.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Jografia* ni elimu ya uso wake dunia.

Dunia imeviringana kama chungwa.

Dunia mara inakwitwa *inchi*, na mara *ulimwengu*.

*Dunia* inayo inchi na maji.

Ni *Planeto* ao *Nyota*, na kama nyota zilizosalia, hai kitu chini yake.

Dunia huenda kwa ginsi mbili,—

Kuzunguka katika jua.

Kugeuka kama pia ichezapo.

## II.

S. Utaniambia nini tena ya kwenda kwake dunia? J.

Dunia hugeuka katika saa asharini na nne, ndio mwendo wake wa siku, na sababu ya kuwa mchana na usiku.

S. Mwendo wa siku wafanyaje mchana na usiku?

J. Sehemu ya dunia iliyogeuka kwa jua yapata nuru, ndio mchana. Sehemu iliyogeuka isilekee jua ina giza, ndio usiku. Dunia ikigeuka, killa sehemu yapata nuru yapata tena giza.

S. Ikiwa nuru ao mchana mahali pamoja pa dunia, ita kuwa na giza ao usiku panginepo?

J. Ndiyo, na baadaye, nikizidi kujua Jografia, nitapata kusema saa ngapi mahali po pote pa dunia.

S. Mwendo wa pili wa dunia unakwitwa nini?

J. Mwendo wa mwaka mzima kulizunguka jua.

S. Mwendo huu wafanya nini?
J. Wakati—Musimu, Masika, Kipupwe, Demani.

### MANENO YA KUKUMUBKWA.

*Mwendo wa siku* wa dunia ndio sababu ya mchana na usiku.

Dunia ikigeuka mchana hufuata usiku, na usiku hufuata mchana mahali pote pa dunia.

Nussu ya dunia ikiwa na nuru, nussu ya pili ina giza wakati uleule.

*Mwendo wa mwaka*.wa dunia, ndio mwendo wa kulizunguka jua.

Mwendo wa mwaka hufanya wakati. *Musimu, Masika, Kipupwe. Demani.*

## III.

S. Tupateje kujua kama dunia imeviringana?
J. Merikebu ikitoka pwani haiishi kuonekana yote pamoja. Sehemu iliyo chini haionekani kwanza, na ncha za milingote zinaonekana mwisho. Bassi kama inchi ingalikuwa sawa, tungaliiona merikebu yote hatta kwisha kuiona kabisa.
S. Nini tena iliyoonya kama dunia imeviringana?
J. Ukienda baharini katika merikebu, utaona kama pwani haionekani kwanza, tena nyumba, tena vilima, na mwisho milima iliyo mirefu sana.
S. Nini tena?
J. Mwezi ukipatwa, giza iliyoonekana juu ya mwezi ni kivuli chake dunia, nacho kimeviringa.
S. Nini tena?
J. Tumesema kama dunia ni planeto ao nyota, bassi nyota zote tunazoziona zimeviringana, hivi na dunia.
Tena kama dunia haingaliviringana ingalikuwa siku zote

mchana upande huu, na sikuzote usiku upande wa pili, lakini twajua kama sivyo.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

Twajua kama dunia imeviringana, kwa sababu—

Merikebu zikitoka pwani, ncha za milingote ndizo zilizoonekana mwisho.

Tukienda baharini, pwani ndiyo tusiyoiona kwanza tena vilima.

*Kivuli* chake dunia *kimeviringa*.

Kama dunia hangaliviringana, upande mmoja ungali kuwa sikuzote na nuru na upande wa pili sikuzote giza.

S. Dunia ni kubwa?

J. Ni kubwa sana. Ukijaribu kusafiri upate kuizunguka, kwenda killa siku mayili kumi utataka kama miaka saba kufika ulikotoka. Urefu kuizunguka ndio mayili ashari na tano elfu.

S. Maana ya kivimba cha dunia nini?

J. Kivimba cha dunia ndicho urefu wa kamba itosha kuizunguka pia.

S. Urefu wa kupenya katika dunia nini?

J. Ndio kipenya chake ao cheo cha kati. Ukiweza ku chimba shimo, na kuchimba na kuchimba, utatoka halafi kwa upande wake wa pili. Shimo lile lingekuwa refu mayili elfu nane, ndio urefu wa kipenya chake.

S. Ekwatori nini?

J. Ekwatori ni kama mstari uliopigwa kuzunguka kati ya dunia, kuiandika nusu kwa nusu Ha pana mstari kama huu, lakini Ekwatori ni mahali mstari huu ungalipitapo.

S. Madara ni nini?

J. Madara ni kama mstari uliopenya katika kati ya dunia. Dunia ikigeuka, mstari huu ndio usiotoka mahali pake, mfano wa mti kati.

S. Poli ni nini?

J. Mapoli ndiyo miisho ya madara, moja linakwitwa Poli la Kaskazini, na moja Poli la Kusini.

MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Kivimba* cha dunia (ao urefu wa kuizunguka) ndicho mayili kama asharini na tano elfu.

*Kipenya* ao urefu wa kati wa dunia ni mayili kama elfu nane.

*Ekwatori* ni mstari uliothaniwa umepigwa kuizunguka dunia katikati.

*Madara* ni mstari uliothaniwa umepigwa kupenya dunia katikati.

Miisho ya Madara inakwitwa—

*Poli la Kaskazini.*

*Poli la Kusini.*

V.

S. Dira ni nini?

J. Dira kitu kama saa, inatumiwa baharini kuonyesha njia ipitayo merikebu.

S. Yapataje kuonyesha?

J. Iko katika dira kama sindano inayogeuka sikuzote kwa Poli la Kaskazini; hivi baharia huona sikuzote kama wanakwenda Kaskazini ao sivyo.

S. Kuna Mapoli ya Magaribi na Mashariki?

J. Hapana, ni Mapoli mawili tu, kwa sababu madara haiwezi kuwa na ncha illa mbili tu.

S. Mashariki na Magaribi ni nini?

J. Mashariki ndiko panapotoka jua, Magaribi ndiko pa-

napozama.

S. Nipateje kujua njia pasipo dira?

J. Kwa jua. Ukitazama panapotoka jua uso wako utalekea Mashariki, Magaribi itakuwa nyuma yako, Kusini kwa mkono wa kuume, na Kaskazini mkono wa kushoto

S. Ziko ishara za kutuonyesha usiku upande gani tunaolekea?

J. Kuna nyota nyingi, na mtu akitazama atajua nyota hizi sikuzote Kusini, na nyota hizi sikuzote Kaskazini ataona tena kama nyota zote hutoka Mashariki huzama Magaribi.

MANENO YA KUKUMBUKWA.

Ncha za dira zilizo kuu ndizo *Kaskazini*, *Kusini*, *Mashariki*, na *Magaribi*.

Dira ni chombo kinachotumika baharini, sindano yake inalekea sikuzote Kaskazini.

Jua latuonyesha ncha zilizo kuu.

Jua hutoka sikuzote katika Mashariki, huzama katika Magaribi.

Kama Kaskazini hulekea Kusini, hivi na Mashariki hulekea Magaribi.

## VI.

S. Ramani nini?

J. Ramani ni kama sanamu ya uso wa dunia. Ukiweza kupaa sana utaona inchi kama katika ramani.

S. Nikitazama ramani sijui maana yake.

J. Hii ndiyo ramani ya dunia; nitajaribu kuifasiri. Wajua kama dunia imeviringana kama chungwa. Tukikata chungwa nussu kwa nussu, vipande vitaonekana kama maviringo haya mawili. Yanakwitwa Hemisfere.

S. Maana ya *hemisfere* nini?

J. *Sfere*, maana yake kiviringana kama tufe. Maana ya *hemi* ndiyo nussu.

S. Maviringo haya yanayo majina?

J. Hili linakwitwa Hemisfere ya Mashariki, na hili Hemisfere ya Magaribi.

S. Mahali pale penyi rangi maana yao nini?

J. Paonyesha inchi na sehemu kubwa zilizo katika dunia. Europa, Asia, Afrika, na Australia ni katika Hemisfere ya Mashariki. Amerika na New Zealand [Nyu Ziland] ni katika Hemisfere ya Magaribi.

S. Tupateje kujua ncha za dira katika ramani?

J. Upande ulio juu ndio Kaskazini, nao ulio chini Kusini. Upande uliolekea mkono wa kuume ni Mashariki na upande wa kushoto ndio Magaribi.

S. Mistari ile ipitayo juu hatta chini, na upande hatta upande, maana yao nini?

J. Yafaa kupima na kupambanua mahali mahali. Ile toka juu hatta chini, ni mistari ya urefu, na ile ya upande hatta upande mistari ya upana.

S. Maana ya urefu nini?

J. Urefu ni cheo cha kuwa mbali kwa Mashariki ao kwa Magaribi. Tukienda Mashariki, ao Magaribi urefu wa mahali petu umebadilika.

S. Upana nini?

J. Upana ni cheo cha kuwa mbali ya Ekwatori kwa Kaskazini ao kwa Kusini. Tukienda Kaskazini ao Kusini, upana wa mahali petu umebadilika.

## MANENO YA KUKUMBUKWA.

Upande wa juu wa ramani ni Kaskazini.

Upande wa chini wa ramani Kusini.

Upande wa ramani uliolekea mkono wa kuume ni Mashariki.

Upande wa ramani uliolekea mkono wa kushoto ni M garibi.

Urefu ni kuwa mbali ya mahali palipochaguliwa kw Mashariki ao kwa Magaribi.

Upana ni kuwa mbali ya Ekwatori kwa Kaskazini a kwa Kusini.

## VII.

S. Katika dunia kuna mahali pa hari na mahali pa baridi
J. Hari na baridi zinafuata upana wa mahali po pote.
S. Pawapi hari?
J. Karibu na Ekwatori.
S. Pawapi baridi?
J. Katika Mapoli.
S. Saa ya mchana ao usiku hufuata upana wa mahali
J. Siyo. Hari na baridi hufuata upana, saa yafuata refu.

S. Mahali palipo mbali panayo saa moja.

J Mahali pote penyi urefu mmoja panayo saa moja Tofauti ya urefu ndiyo sababu ya tofauti ya saa.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

Sehemu ya dunia panapo hari nyingi ndiyo iliyo karibu na Ekwatori.

Sehemu za dunia panapo baridi nyingi ndizo zilizo karibu na Mapoli.

Sehemu za dunia pasipo hari nyingi mno, wala baridi nyingi mno, ndizo zilizo katikati ya Mapoli na Ekwatori.

Saa yafuata urefu wa mahali.

Ikiwa athhuuri hapa, saa ileile imekuwa nussu ya usik upande wa pili wa dunia.

## VIII.

S. Maana ya uso wa dunia nini?

J. Uso wa dunia ni upande wa juu au upande wa nje. ndio upande ulioonekana. Jografia ni elimu ya uso wa dunia. Elimu ya vitu vilivyo ndani mwake elimu nyingine.

S. Sehemu za inchi zinakwitwaje?

J. Kontinenti, Visiwa, Penisula, na zinginezo.

S. Maana ya Kontinenti nini?

J. Kontinenti ni sehemu ya inchi ilivo kuu.

S. Makontinenti mangapi yanayo?

J. Kuna Makontinenti matano.

S. Nambie majina yao.

J. Europa, Asia, Afrika, Amerika, na Australia.

S. Mangapi yaliyo katika Hemisfere ya Magaribi?

J. Amerika peke yake.

MANENO YA KUKUMBUKWA.

Uso wa dunia ndio upande wa nje.

Sehemu ya inchi iliyo kuu inakwitwa *Kontinenti*.

Kuna *Makontinenti* matano, Europa, Asia, Afrika, Amerika, na Australia.

Amerika ni katika Hemisfere ya Magaribi.

## IX.

S. Kontinenti ni inchi moja tu?

J. Katika Kontinenti hupambanua ufalme fullani fullani, inchi ya taifa ao kabila hii na hii.

S. Kuna sehemu tena baada ya Kontinenti?

J. Sehemu ya inchi iliyozungukwa na maji ni Kisiwa.

S. Ikiwa karibu ya kuzungukwa tu?

J. Yaitwa Penisula.

S. Nitajie inchi zilizo katika Kontinenti ya Afrika.

J. Uyao, Unyamwezi, Misri.

S. Nitajie visiwa.

J. Unguja, Pemba, Mafya, Buki.

S. Makontinenti hayakuzungukwa na maji? .

J. Yamezungukwa, lakini makubwa sana. Europa Asia, na Afrika, yangalikuwa kisiwa kimoja, na Amerika kimoja, na Australia kimoja.

S. Kontinenti lipi lililo dogo?

J. Ndilo Australia, zamani limekwitwa kisiwa kilicho kikubwa.

S, Nitajie Penisula?

J. Mji wa Unguja, Rasi Hafuni, Arabuni.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

Makontinenti yanayo inchi nyingi.

*Inchi* ni sehemu ya Kontinenti, kama Uyao katika Afrika, na Arabuni katika Asia.

*Kisiwa* ni sehemu ya inchi ndogo iliyozungukwa na ma' kama Unguja na Pemba.

*Penisula* ni sehemu ya inchi iliye karibu kuwa kisiwa, kama Rasi Hafuni iliyo ndogo, na Arabuni iliyo kubwa.

## X.

S. Isimusi ni nini?

J. Isimusi ndiyo shingo la inchi iliyounga sehemu mbili yake. Isimusi ya Suwes yaunga Asia na Afrika. Isimusi ya Panama yaunga Amerika ya Kaskazini na Amerika ya Kusini.

S. Rasi ni nini?

J. Rasi ni ncha kama pua ya inchi itokayo katika bahari, kama Rasi Kizimkazi.

S. Maana ya pwani nini?

J. Inchi ifikapo baharini.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Isimusi* ni shingo la inchi iungayo sehemu mbili. kama

Isimusi ya Suwes kati ya Asia na Afrika.

*Rasi* ni ncha ya inchi itokayo katika bahari, kama Rasi Kizimkazi.

*Pwani* ndiyo inchi iliyo karibu na bahari.

## XI.

S. Tofauti gani ya kilima na mlima ?

J. Mlima ni mkubwa sana, kilima ni kidogo tu.

S. Milima iliyo mirefu sana iko wapi ?

J. Iko katika Asia na Amerika.

S. Milima yafaa nini ?

J. Hukusanya mawingu, hunyesha mvua nyingi, ndio asili ya mito ya maji.

S. Milima yafaa nini tena ?

J. Hupambanua mipaka ya inchi, hugeuza tabia ya inchi zilizo karibu nao.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Mlima* ni kilima kilicho kikubwa sana, kama Kilimanjaro.

Milima iliyo mikubwa sana iliyoko katika Asia na katika Amerika.

Milima hufanya mipaka ya inchi na mataifa.

Milima ndiyo asili ya mito ya maji.

## XII.

S. Maana ya Delta nini ?

J. Delta ndiyo inchi ya chini iliyo katika mito mingi mikubwa iingiapo baharini; kama Delta ya mto Nil na Delta ya mto Lufiji.

S. Maana ya Pleni nini ?

J. Pleni ndiyo inchi iliyo sawa haina vilima wala haina

boonde. Pleni ikiwa juu sana kuliko bahari yaitwa **Plato ao** Meza ya inchi.

S. Maana ya Deserti nini?

J. Deserti ndiyo jangwa, ao pleni pasipo maji.

S. Volkano ni nini?

J. Volkano ni mlima wa moto. Hutoka kwake moto na moshi na majifu na maadini iliyoyeyuka. Angazidja na Kenya ni mavolkano.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Delta* ni inchi yenyi maji iliyoko mito iingiapo baharini

*Pleni* ni inchi pana na sawa.

*Plato* ao *Meza ya inchi* ni pleni iliyo juu sana kuli bahari.

*Boonde* ni inchi ya chini iliyo katikati ya vilima.

*Deserti* ni pleni pasipo maji.

*Volkano* ndilo mlima wa moto.

## XIII.

S. Sehemu za maji zilizo kubwa, zaitwaje?

J. Maokeani, na kama yanayo Makontinenti matano, yako na Maokeani matano.

S. Nambie majina yao.

J. Maokeani matano ndiyo la Hindi, Atlantiko, Pasifiko, Arktiko (la Kaskazini), Antarktiko (la Kusini).

S. Yako wapi Maokeani haya?

J. Lile la Hindi ni kati ya Afrika na Australia. Lile Atlantiko ni kati ya Europa na Afrika upande mmoja na Amerika upande wa pili. Lile Pasifiko ni kati ya Amerika upande mmoja na Asia na Australia upande wa pili. Lile Arktiko lazunguka Poli la Kaskazini. Lile Antarktiko lazunguka Poli la Kusini.

S. Tofauti gani ya Okeani na bahari?

J. Bahari ni ndogo kuliko Okeani, kama Bahari ya Sham.

MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Maokeani* ndiyo sehemu za maji zilizo kubwa.
Maokeani matano ndiyo—
*La Hindi*, kati ya Afrika na Australia.
*Atlantiko*, kati ya Europa na Amerika.
*Pasifiko*, kati ya Amerika na Asia.
*Arktiko*, karibu na Poli la Kaskazini.
*Antarktiko*, karibu na Poli la Kusini.
*Bahari* ni sehemu ya maji iliyo ndogo kuliko Okeani.

S. Mlango wa maji ni nini?

J. Mlango wa maji ndiyo sehemu nyembamba ya maji kati ya bahari mbili, kama mlango wa Bab el Mandeb kati ya Bahari ya Sham na Bahari ya Arabuni.

S. Ghubba ni nini?

J. Ghubba ni sehemu ya maji iingiayo katika inchi kwa namna ya tao. Ikiwa ndefu na nyembamba yaitwa Hori.

S. Bandari ni nini?

J. Bandari ni mahali pa baharini pasipofika mawimbi makuu kwa sababu ya inchi ao visiwa.

MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Mlango* ndiyo sehemu nyembamba ya maji kutoka bahari hii kuingia bahari ile.

*Ghubba* ni sehemu ya bahari iingiayo katika inchi.

*Hori* ni Ghubba iliyo ndefu na nyembamba.

*Bandari* ni mahali merikebu zitiapo nanga pasipo hatari ya mawimbi.

S. Ziwa la maji ndilo nini ?

J. Ziwa ni sehemu ya maji iliyozungukwa na inchi.

S. Maji ya ziwani ni maji ya chumvi, ao maji ya baridi ?

J. Ziwa likiwa kubwa na maji yake ya chumvi, huitwa Bahari, kama Bahari Kaspiani. Maji yake yakiwa mata ... ta'twa sikuzote Ziwa.

S. Yako wapi Maziwa yaliyo makubwa ?

J. Yako katika Amerika, yako tena katika Afrika, ka ... Nyassa, Tanganyika, na Nyanza.

MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Ziwa la maji* ni maji yaliyozungukwa na inchi.

Maziwa yenyi maji ya baridi yaliyo makubwa ni katika Amerika na katika Afrika.

Ziwa lililo kubwa sana ni Bahari Kaspiani, lakini ma... yake yana chumvi.

## XVI.

S. Mto wa maji nini ?

J. Mto wa maji ndio maji yatokayo katika milima, ao mahali pa juu, yashukayo kwenda baharini.

S. Mito yapataje kutoka milimani.

J. Milima hukusanya mawingu, mawingu huunyesha mvua, maji ya mvua hupita katika inchi hatta mahali panapozibwa, hutoka tena kwa chemchemi. Katika chemchem' hutoka vijito, vijito vikifikana hufanya mto.

S. Kinwa cha mto nini ?

J. Kinwa ndipo panapoingia maji ya mtoni katika bahari. Mto ufikao baharini kwa vinwa vingi hufanya Delta, ndiyo inchi iliyo kati ya vinwa vyake.

S. Mwanzo wa mto nini ?
J. Ndio utokako katika inchi.

### MANENO YA KUKUMBUKWA.

*Mto* ni maji yaendayo baharini.
*Mwanzo wa mto* ndio utokako katika inchi.
Mwanzo wa mto ni mlimani ao pahali pa juu sana.
*Mwisho wa mto* ndio uingiapo baharini.
Mito iliyo mikubwa ndiyo Nil na Kongo katika Afrika. na Misisippi na Amazoni katika Amerika.

UNIVERSITIES' MISSION PRESS, ZANZIBAR.